BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Nne – Tarehe 02 Disemba, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa mwaka 2023/2024.

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) kwa mwaka 2023/2024.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Taarifa ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda juu ya Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa mwaka 2023/2024.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Taarifa ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda juu ya Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) kwa mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

77. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Nazipongeza juhudi za viongozi wakuu wa nchi yetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mama Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala kwa lengo la kuhifadhi mazingira.

(a) Je, Wizara yako imeshafanya tathmini ili kujua kwa asilimia ngapi Wazanzibari wanatumia nishati safi ya kupikia.

(b) Kwa kuzingatia matarajio ya Wizara yako, ni asilimia ngapi ya watumiaji wa nishati mbadala itakuwa imefikiwa hadi kufikia Disemba 2025.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

120. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Idara ya Usalama na Afya Kazini ni muhimu kwa maendeleo ya nchi. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa Idara hiyo bado inaonekana kutofanya kazi kwa ufanisi, jambo ambalo linapelekea Serikali kukosa mapato mengi kutokana na sheria zilizopitwa na wakati na ukosefu wa mamlaka kwa Idara hiyo.

(a) Je, ni lini Serikali itaifanyia marekebisho sheria husika na kuifanya Idara hiyo kuwa mamlaka kamili.

(b) Je, Serikali hupata kiasi gani cha mapato kutokana na malipo ya huduma zinazotolewa na Idara hiyo kwa mwaka.

(c) Je, ni vikwazo vipi vinavyoifanya Idara hii kushindwa kuwa mamlaka inayoweza kuisaidia nchi katika maendeleo.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

129. MHESHIMIWA CHUM KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wawanake): Atamuuliza Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Awamu ya nane imeamua kujenga masoko katika nchi nzima kupitia Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya.

Je, kuna mpango gani wa Serikali kwa yale maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma hii.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

4. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hivi karibuni kumeibuka changamoto ya kuadimika kwa fedha za kigeni hasa Dola za Marekani.

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kukabiliana na changamoto hii.

11. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika kipindi cha hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la taasisi binafsi za ukaguzi wa mahesabu (Auditing Firms) hapa Zanzibar. Pamoja na kazi kubwa zinazofanywa na ‘Auditing Firms’ hizi, bado zinakabiliwa na changamoto ikiwa ni pamoja na kutambulika kwake na kupelekea ongezeko la vishoka katika sekta hii ya ukaguzi.

(a) Je, kwa takwimu ni taasisi ngapi za ukaguzi (Auditing Firms) zimesajiliwa nchini kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu.

(b) Je, ni yepi majukumu ya Bodi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi (ZIAAT) katika kuzisimamia ‘Auditing Firms’ zilizopo Zanzibar.

(c) Je, ni yepi mashirikiano baina ya Bodi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi (ZIAAT) na Bodi ya Wahasibu ya Tanzania Bara (NBA).

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

98. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuona umuhimu wa kujenga Skuli kubwa ya kisasa ya Chukwani, ingawa muda tulioahidiwa kukamilika kwa ujenzi wake umeshapita.

Ni changamoto gani iliyopelekea kutokamilika kwa ujenzi huo mpaka sasa.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

34. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tathmini ya maendeleo ya kukua kwa soka la Zanzibar iko vipi kwa sasa.

35. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Michezo mingi ya asili ya watoto wa kizanzibari ilikuwa na maana na mantiki kubwa kwa jamii.

(a) Ni zipi athari hasi za kiutandawazi zilizopelekea kupotea michezo ya asili ya watoto wetu.

(b) Kuna tofauti gani iliyopo kijamii na kimaadili kwa michezo ya asili ya watoto wa kizanzibari katika kipindi hiki cha utandawazi.

**Wizara ya Afya:**

23. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazoongoza barani Afrika kuwa na huduma za karibu sana za vituo vya afya.

Je, ni yepi matarajio ya wananchi kupitia Wizara yao juu ya kuwapatia huduma bora zaidi za kimatibabu hususani kwa maradhi yasiyoambukiza.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

67 MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni utaratibu gani unaotumika kujisajili rasmi vijiwe vya bodaboda.

68. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

(a) Kuna aina ngapi za namba za msingi za dharura ambazo wananchi wanatakiwa wazifahamu na kuzitumia inapotokezea haja ya kufanya hivyo.

(b) Muitikio uko vipi juu ya uelewa na ufuatiliaji wa karibu sana katika kuweza kutatua changamoto mbali mbali zinazowakabili wananchi wetu kupitia namba za msingi na za dharura.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

15. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wizara yako iliahidi kuongeza idadi ya mifumo ya umwagiliaji maji ili kuwasaidia wakulima kuondokana na kilimo cha mazoea.

(a) Je, kwa hivi sasa hali ipo vipi.

(b) Ni asilimia ngapi ya wakulima wanaokosa huduma ya mifumo ya umwagiliaji maji.

(c) Nini matarajio halisi ya Serikali katika kuyafikia malengo yaliyokusudiwa.

110. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Sensa ya miti (wood biomass survey) ni nyenzo muhimu ili kufahamu mabadiliko ya uoto wa asili, wingi wa misitu tuliyonayo na idadi ya mikarafuu. Hadi sasa, Zanzibar haijafanya jumla ya sensa 5 zinazohusiana na masuala ya miti, ambayo ni

muhimu ili kubaini miti iliyoko katika hatari ya kutoweka na kuweka mkazo katika kuilinda.

(a) Je, ni ipi tathmini ya sensa ya miti iliyopo hivi sasa kwa uoto wa asili, misitu na mikarafuu.

(b) Je, upi muongozo wa kitaifa na kimataifa katika kufanyika sensa ya miti katika nchi.

(c) Je, ni changamoto zipi ambazo Serikali imekumbana nazo hadi kushindwa kufanya sensa hii ya miti.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

52. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Je, sheria ziko vipi juu ya suala zima la ulinzi wa wazee.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

59. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Kwa kiasi gani Wizara yako inatoa msukumo katika taasisi mbali mbali ikiwa ni pamoja na taasisi maarufu ya 'Karibu Zanzibar Festival' katika kukuza utalii nchini.

(b) Je, ni juhudi zipi Wizara inazozichukua katika kuongeza vivutio vya utalii nchini.

60. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Ni lini Serikali itaikarabati 'Majestic Cinema' ili iweze kutumika kama ni moja ya vyanzo muhimu vya kihistoria na utalii Zanzibar.

## III. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa mwaka 2023/2024

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) kwa mwaka 2023/2024

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**02 Disemba, 2024.** **KATIBU WA BARAZA.**